## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA KUMI NA NANE

**28 APRILI, 2021**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA TATU

**KIKAO CHA KUMI NA NANE – TAREHE 28 APRILI, 2021**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MADINI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha

2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

## III. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**148. MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS KAMOLI (SEGEREA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

(a) Je, ni lini Serikali itaongeza Vituo vya Afya katika Kata za Jimbo la Segerea pamoja na kupandisha hadhi Zahanati za Kinyerezi, Segerea, Kipawa na Yombo Kiwalani ili kuondoa adha kwa Wananchi wa Kata 13 wanaotegemea Kituo kimoja cha Afya;

(b) Je, ni lini Kata za Minazi Mirefu, Buguruni, Kimanga na Kisukuru zitapatiwa Zahanati.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**149. MHESHIMIWA MWANAKHAMIS KASSIM SAID (MAGOMENI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa waliokuwa Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano waliostaafishwa kwa maslahi ya Umma Tarehe 30 Juni, 1996.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**150. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Wananchi wanaoishi jirani na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro Wilayani Karatu kwa muda mrefu wamekuwa wakipata adha kubwa ya Wanyama kuingia na kuvamia mashamba yao na wakati mwingine kujeruhi Wananchi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo hilo.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**151. MHESHIMIWA JAFFAR SANYA JUSSA (PAJE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itavipatia Vituo vya Polisi vya Paje na Jambiani samani za Ofisi pamoja na magari kwa ajili ya doria.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**152. MHESHIMIWA ROSE CYPRIAN TWEVE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha utaratibu maalum wa kuvuna viungo vya binadamu kama vile Figo na Moyo kwa ajili ya Watanzania wenye uhitaji wa viungo hivyo.

**153. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Mwaka 2018 KFW Germany walisitisha udhamini kwa huduma za Afya kwa Mama na Mtoto Mkoani Tanga.

(a) Je, ni juhudi gani zimefanyika kuhakikisha Mdhamini huyo anaendelea na udhamini wake Mkoani Tanga;

(b) Je, Serikali ina mpango gani kupata Mdhamini mwingine.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**154. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Tingi – Kipatimu yenye urefu wa Km 50 kwa kiwango cha lami hasa ikizingatiwa kuwa barabara hiyo inapita katika maeneo yenye kumbukumbu za Vita vya Majimaji na vivutio muhimu vya Utalii.

**155. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Daraja kwenye Mto Malagarasi ili kuunganisha Kata ya Ilagara na Kata ya Sunuka katika Wilaya ya Uvinza.

**WIZARA YA KILIMO:**

**156. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kufufua zao la Kahawa nchini ambalo ni moja ya mazao ya kimkakati;

(b) Je, ni lini Makampuni binafsi yataruhusiwa kununua Kahawa kwa Wakulima moja kwa moja bila kupitia Vyama vya Ushirika.

**157. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha uzalishaji wa zao la Vanila nchini.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**DODOMA** **S. KAGAIGAI**
**28 APRILI, 2021** **KATIBU WA BUNGE**